# e-GA tupo tayari kushirikiana na sekta binafsi

**Na Zena Mohamed, Dodoma**

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (e-GA), imeahidi kushirikiana na Benki ya NMB kuimarisha, kukuza na kuendeleza ujuzi na vipaji kwa vijana wa Kitanzania wabunifu na wale wanaosoma fani ya TEHAMA katika Vyuo Vikuu mbalimbali nchini, kupitia programu maalum ya mafunzo kwa vitendo inayotolewa na e-GA kupitia Kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC).

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Benedict Ndomba, wakati wa kikao cha pamoja kati ya e-GA na Benki ya NMB kilichofanyika katika Makao Makuu ya ofisi za e-GA jijini Dodoma.

Kikao hicho kililenga kujadili namna taasisi hizo zinavyoweza kushirikiana katika maeneo mbalimbali ya teknolojia.

Maeneo hayo ni pamoja na utafiti, matumizi ya teknolojia za kisasa, kuvumbua vipaji na kuviendelea kwa vijana wabunifu wa Kitanzania, pamoja na kutoa fursa kwa vijana wavumbuzi na wabunifu ikiwa ni sehemu ya kuendeleza Sekta ya TEHAMA nchini.

Ushirikiano huo unatarajiwa kuongeza na kukuza fursa za ajira kwa vijana sambamba na kuimarisha uhusiano mzuri kati ya Serikali na sekta binafsi kwenye eneo la TEHAMA, alisema Ndomba .

"e-GA imekuwa ikishirikiana na Vyuo Vikuu mbalimbali nchini katika kuwapata vijana wenye ujuzi, hivyo makubaliano hayo kati ya e-GA na NMB ni muendelezo wa ushirikiano mzuri uliopo kati ya e-GA na wadau mbalimbali wa TEHAMA", alifafanua Ndomba.

Aliongeza kuwa katika kikao hicho taasisi hizo zimekubaliana kushirikiana na kuandaa mkataba wa makubaliano (MOU) ambapo baada ya kukamilika kwa mkataba huo, pande zote mbili zitakutana na kujadiliana namna ya utekelezaji wa makubaliano hayo.

"e-GA imekuwa ikiwatengeneza vijana wanaoshiriki programu maalum ya mafunzo kwa vitendo pamoja na utaratibu wa kujitolewa (interns and volunteering) kupitia kituo chetu cha utafiti na ubunifu, kwa kuwajengea uwezo zaidi ili kwenda sambamba na soko la ajira pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoibuka kila siku", alisema Ndomba.

Aidha, Ndomba aliishukuru Benki ya NMB kwa kuona umuhimu wa kutengeneza wataalamu wazawa wa TEHAMA kupitia programu hiyo na kuwa, e-GA ipo tayari kushirikiana na benki nyingine zenye dhamira ya kuijenga Tanzania ya kidijitali katika sekta zote za serikali na binafsi.

Naye Meneja eGovRIDC Dkt. Jaha Mvulla alisema, e-GA ipo tayari kushirikiana na Benki ya NMB katika maeneo mbalimbali yanayolenga kukuza matumizi ya TEHAMA nchini ikiwemo eneo la rasilimali za miundombinu na vifaa vya TEHAMA vya kufanyia mazoezi na majaribio, ubunifu hasa maeneo ya teknolojia mpya, kujenga uwezo na uzoefu kwa vijana, mafunzo kwa vitendo, utafiti na machapisho, maonesho, mashindano mbalimbali ya kidigitali kwa ajili ya kuvumbua vipaji, na maeneo mengine yanayohusiana na jitihada za Serikali Mtandao na teknolojia za kifedha.

"e-GA ipo tayari kufanya kazi na NMB kupitia programu maalumu ya mafunzo kwa vitendo inayoendeshwa na eGovRIDC, ili kuchochea ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya zinazoibuka duniani ikiwemo Akili Bandia (AI), Machine Learning, Blockchain na matumizi yake kama vile kujenga ulewa wa teknolojia kama za Digital Currency na FinTech, Utengenezaji wa mifumo (System Development) kwa ajili ya kutatua changamoto zetu nchini na usalama mtandaoni (Cyber Security)", alisema Dkt.Jaha.

Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu- Kituo cha Taaluma NMB Bi. Joanitha Rwegasira alisema kuwa, Benki ya NMB imeandaa programu hiyo ili kuongeza idadi ya vijana wabobezi kwenye masuala ya TEHAMA watakaofanya kazi katika sekta za umma na binafsi kwa lengo la kukuza taifa la kidijitali.

Programu hiyo itasaidia kufanya majaribio ya teknolojia mpya zinazoibuka ikiwemo Sarafu ya mtandaoni na kutoa suluhu kwenye maeneo mbalimbali yenye changamoto katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi ikiwemo matishio ya usalama mtandaoni, ubunifu wa mifumo n.k, alisema Rwegasira

Aidha, aliishukuru Mamlaka kwa kuonyesha utayari wa kushirikiana na NMB na kwamba watatumia fursa hiyo katika kuhakikisha wanaboresha huduma za kibenki hususani huduma zinazotolewa kidijitali.



Katibu wa Kamati Maalum ya NEC, Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, akikagua jengo la wanafunzi wa kike lililoungua kwa ajali ya moto katika skuli ya sekondari ya Hasnuu Makame iliyopo Wilaya ya Kusini Unguja mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu)

# SMZ kukarabati mabweni yaliyoungua

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

KATIBU wa Kamati Maalum ya NEC,Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar,Khamis Mbeto Khamis amesema CCM itaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuharakisha ukarabati wa mabweni ya wanafunzi iliyoungua moto hivi karibuni katika Skuli ya Sekondari ya Hasnuu Makame,iliyopo Wilaya ya Kusini Unguja.

Kauli hiyo ameitoa jana katika ziara yake ya kutembelea na kukagua Skuli hiyo huko Wilaya ya Kusini Unguja,amesema Chama Cha Mapinduzi kinatoa pole kwa uongozi wa wilaya hiyo pamoja na wanafunzi kwa ujumla na kuwasihi waendelee kuwa wavumilivu katika wakati huu ambao Chama na Serikali wanaendelea kutafuta ufumbuzi wa kufanya ukarabati na kurejesha huduma mbalimbali skulini hapo.

Mbeto,amewasihi viongozi wa Wilaya hiyo kufanya juhudi binafsi za kuhakikisha wanafunzi wote wanaendelea na masomo hasa wale waliopo katika kambi kwa ajili ya maandalizi ya mitihani ya kidato Pili na Nne ili waendelee kupata huduma za kielimu.

"Chama Cha Mapinduzi kimepokea kwa masikitiko taarifa za ajali hii ya kuungua kwa moto nyumba ya kulala wanafunzi wetu wa kike katika Skuli ya Hasnuu Makame, tunaahidi kuendelea kushirikiana nanyi katika kuchukua hatua za haraka Ili wanafunzi waendelee na masomo yao.",alisema Mbeto.

Katika maelezo yake Mbeto,ameahidi kuwa CCM itatoa mchango ili kuunga mkono juhudi za kuhakikisha wanafunzi wa Skuli wanaendelea kupata elimu bora.

Akizungumza Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja Rajab Mkasaba,alisema ajali hiyo ilitokea Octoba 12,mwaka 2023 majira ya usiku wa saa 2:00,na chanzo cha moto huo inasadikika kuwa itilafu ya umeme.

DC.Mkasaba,alisema Serikali inaendelea na juhudi za kufanya tathimini kwa ajili ya kujua gharama halisi za matengenezo hayo ili kuhakikisha jengo hilo linatengenezwa na wanafunzi wanaendelea na masomo.

Aliwaomba wadau wa maendeleo ,wafanyabiashara maarufu pamoja na watu wenye uwezo kutoa michango ya kusaidia Skuli hiyo ili iweze kumudu gharama mbalimbali za mahitaji ya wanafunzi hao ambao vifaa vyao vyote viliungua kwa moto.

Naye Mwalimu Mkuu wa Skuli hiyo,Bakar Mohamed Ali,alisema kwa makisio ya awali vifaa vya wanafunzi na Skuli vilivyoungua moto vinagharimu kiasi cha milioni 115.

Nyumba hiyo ya kulala wanafunzi wa kike ilikuwa na vyumba 13 na vyoo 10 ambapo jumla ya wanafunzi 135.

# Wananchi wengi zaidi kupata maji

**Na Mwandishi Wetu, Tabora**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Igunga (IGUWASA) imehitimisha wiki ya huduma kwa mteja na kuvutia wadau mbalimbali na wananchi katika utoaji wa huduma.

Wiki hiyo ambayo ilizinduliwa rasmi Oktoba 1.2023 na kuhitimishwa Oktoba 1, 2024, ambapo IGUWASA wameongeza wiki moja zaidi hadi tarehe 14.10.2023 siku ya kumbukizi ya Hayati Rais wa Kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, Meneja wa IGUWASA Mhandisi Hamphrey Mwiyobela, alisema maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja "Customer Service Week".

Alisema kwamba, IGUWASA inathamini mchango mkubwa wa wateja wake katika kusaidia kufikia malengo ya kutoa huduma ya maji mjini Igunga, ambayo yameongezeka kwa kasi kubwa na kufikia asilimia 98 ya usambazaji maji kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Katibu Mwenezi, Itikadi na Siasa wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wilaya ya Igunga Peter Kalindo, CCM inaridhishwa na Utendaji kazi wa IGUWASA ikiwa ni taasisi ya Serikali, kwani imekirahisishia ufanyaji wa kazi.

"Upande huo wa Ilani unazungumzia habari ya maji, ambapo chama kimeelekeza kupitia Ilani kuwa mpaka kufikia mwaka 2025 tunatarajia kwamba huduma za maji vijijini zitakuwa zinapatikana kwa asilimia 85 na mijini kwa asilimia 95, lakini kwa upande wa IGIWASA kwa maana ya mamlaka ya maji hapa mjini Igunga wamefanikiwa na wamevuka lengo la Ilani kwa sababu wao wamehakikisha mpaka sasa kwa habari ya maji mjini wateja wanapata kwa asilimia 98," alisema Kalindo.

Aliendelea kusema, "Tumevuka lengo la Ilani kwa asilimia tatu kwa kutoa huduma nzuri na kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi, baada ya CCM kutangaza kwa wananchi kuwa mkoa wa Tabora umepokea zaidi ya sh. bilioni 600 kwa maana ya Nzega, Igunga na Tabora kwa lengo la kusabaza maji ya Ziwa Victoria hadi kufika hapa wilayani kwetu, hakika kasi ya usambazaji wa huduma ya maji imekuwa ni kubwa sana na wananchi wengi wamevutiwa kwa sababu maji ni uhai, maji huboresha afya na huboresha mazingira."

Kalindo alibainisha kuwa, mpaka sasa bei ya kuunganishiwa maji ni rafiki na imepelekea wananchi wengi kuvuta maji majumbani na kuongeza kasi ya usambazaji na kuyafikia maeneo mengi